# LEARNING BY EAR

# "If a tree falls… - Deforestation in Africa"

## EPISODE NINE: "Sesi's Dark Secret"

**AUTHOR: Romie Singh**

**EDITORS: Thomas Mösch, Jan-Philipp Scholz**

**PROOFREADING: Natalie Glanville-Wallis**

## List of characters EPISODE NINE:

**Narrator**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **SCENE 1** | **Mulogo (m, 22)** | | |
| **SCENE 2** | **Mulogo (m, 22)** | **Chika (f, 18)** | |
| **SCENE 3** | **Talib (m, 20)** | **Chika (f, 18)** | |
| **SCENE 4** | **Mulogo (m, 22)** | **Chief(m, 40)** | |
| **SCENE 5** | **Isi (f, 18)** | **Akiki (f, 7)** | |
| **SCENE 6** | **Mother (m, 36)** | **Mulogo (m, 22)** | **"Themba" (f, 30)** |
| | **Chika (f, 18)** | **Chief (m, 40)** | **Talib (m, 20)** |
| | **Mixed crowd** | | |
| **SCENE 7** | **Chief (m, 40)** | **Isi (m, 18)** | **Sesi (f, 18)** |
| **SCENE 8** | **Akiki (f, 7)** | | |

## INTRO

Karibu kwenye *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* na katika kipindi cha tisa cha mchezo wetu mpya kuhusu uharibifu wa misitu.

Kisa hiki kinaendelea kwenye mazingira ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na kinaonyesha jinsi uharibifu wa misitu- ukataji wa miti na maeneo ya nyasi- ulivyotatiza maisha ya vijijini na kusababisha mzozo kati ya jamii mbili za wakulima. Sasa jamii hizo mbili zinajikuta ziko pamoja kwenye kambi ya wakimbizi ya Dovani na zimeanza kutafuta ufumbuzi sawa kwa matatizo ya siku za usoni.

Je Sesi ana habari gani na je Akiki ana siri nyingine? Kiongozi wa kambi ya wakimbizi ya Dovani, Talib, hana raha. Anataka uhusiano wa karibu zaidi na mwenzake Chika. Lakini Chika anamwambia angependa wasalie kuwa marafiki ya kawaida.

**Episode NINE: "SESI'S DARK SECRET."**

**<u>1. MUSIC UP</u>**

**<u>Scene 1</u>**

**2.MULOGO NARRATOR:** Miezi michache iliyopita nimebadilisha sana mtazamo wangu kuhusu mambo mengine kutokana na kushirikiana na Talib na Chika. Sasa nakubali – uharibifu wa misitu unadhuru mazingira yetu na maisha yetu. Gesi za viwandani zimeongezeka kwa kiasi kikubwa na hivyo kusababisha hali ya hewa ya dunia kubadilika. Miti hufyonza mathalani gesi aina ya “Carbon dioxide”. Kwa hivyo wakulima wanapaswa kuacha tabia ya kukatakata na kuchoma misitu na watafute njia nyingine za kuendesha maisha yao. Ninafahamu kuhusu mafuriko yyanayotokea kwenye mto uliyoko Mlima Elgon, kuyeyuka kwa theluji ya Mlima Kilimanjaro , jinsi Ziwa Chad linavyokauka. Uharibifu wa misitu unatuathiri sote, si Afrika tu bali duniani kote. Nimejifunza mambo mengi kwenye mazungumzo kati yangu na Chika na baada ya mkutano mkubwa wa jana tulikubaliana kuanzisha kundi la usimamizi wa misitu. Nilipata fursa ya kuzungumza naye kwa faragha. Na mambo yakawa yalivyokuwa!

**<u>3.MUSIC UP</u>**

**Scene 2**

**4. SFX Daytime ambience outside**

**5.MULOGO:** Umekuwa mkutano mzuri sana, Chika. Tumeamua kulivalia njuga suala hili vilivyo!

**6.CHIKA:** Naam- lakini hapo awali hukuwa na subira. Mawazo yako mengine yalikuwa ya kiwango cha juu- mtambo wa umeme, bwawa na hifadhi ya maji, Tunataka njia za ufumbuzi ambazo watu wa mashinani wanaweza kuzitekeleza na kuzidhibiti.

**7.MULOGO:** Natumai unasema tunapaswa kuanzia chini kwenda juu badala ya kutoka juu kwenda chini.

**8.CHIKA:** Naam!

**9.MULOGO: (softer tone)** Unafikiri utafanya nini pindi sote tukirudi kwenye jamii zetu?

**10.CHIKA:** Sijui. Na wewe?

**11.MULOGO:** Babangu anataka nipate elimu ya kunifaa. Anafikiri sijakomaa sawa sawa. Nimepinga mawazo yake ya kienyeji kwa muda mrefu. Lakini hata hivyo, siku zote nimekuwa nikimheshimu. Ana kipaji cha uongozi.

**12.CHIKA:** Wazo lake kuhusu jiko limefaulu kupita kiasi!

**13.MULOGO:** Naam na mimi pia nataka kujiendeleza kwenye taaluma ya sayansi, nijiunge na chuo cha kilimo, nijifunze kuhusu kilimo kinachohusisha misitu, nishati mbadala na mambo kama hayo.

**14.CHIKA: (Shocked)** Salala! Utatoweka kwa muda mrefu?

**15.MULOGO: (tenderly)** Kwani nikiondoka utatamani niwepo?

**16.CHIKA: (embarrassed)** Naam. Nadhani hivyo. Tumekuwa na mijadala mizuri..

**17.MULOGO: (intimate)** Hiyo tu ndiyo unayofurahia?

**18.CHIKA: (tenderly)** Mulogo**. (Kiss)** Mulogo!

**19.MULOGO: (soft kisses)** Basi twende tusome pamoja!

**20.CHIKA: (laughing)** Una bidii sana mwanamume wewe!

**21.MULOGO:** Bila shaka. Najua nikitakacho! Mimi ni mwanawe Chifu Apaloo! Na siku moja utakuwa mke wangu!

**<u>22.MUSIC UP</u>**

## SCENE 3

**23. SFX Office ambience (typing, papers)**

**24.TALIB: (feeling shy)** Chika. Natumai hutasikia vibaya nikisema.. kwamba..ee... nakuona siku hizi umebadilika.

**25.CHIKA:** Alaa! Nimebadilika vipi?

**26.TALIB:** Sijui. Tumekuwa tukishirikiana kwenye miradi mingi. Na sasa ninahisi kama ambavyo tunatengana.

**27.CHIKA:** Lakini nimejitolea kwa yote tunayofanya.

**28.TALIB:** Nadhani ninajisumbukia mimi binafsi. Nimekuwa nikikupenda siku zote hizo na nilitumaini kwamba kuna uwezekano wetu sisi kuwa zaidi ya marafiki wa kawaida.

**29.CHIKA: (gently)** Nimekufahamu. Ai Talib! Tuna mambo mengi ya kufanana! Mimi siku zote hukuchukilia kama kakangu!

**30.TALIB: (disappointed)** Alaa! Hayo yananifanya nijihisi kana kwamba hakuna lolote langu linalokufurahisha!

**31.CHIKA: (laughing)** Sivyo. Nikiwa nawe sina wasiwasi wa jambo ninalofanya. Lakini..kweli...sijui niseme nini kuhusu mvuto.

**32.TALIB:** Na unavutiwa na Mulogo! Samahani! Hayo hayanihusu!

**33.CHIKA:** Hapana! Sivyo hivyo. Wajua, kuna vita vinavyoendelea na siku moja vikiisha hakuna ajuaye maisha yetu yatatuelekeza wapi!

**34.TALIB:** Samahani kwa kukutajia hayo.

**35.CHIKA:** Si neno Talib. Nadhani ni vizuri kuwa mkweli. Lakini sasa hivi tuzingatie yanayotukabili! Awamu ya pili. Kuainisha maeneo ya misitu na rasilimali zetu. Jamii zetu zitahitaji uzoefu huu kuhifadhi misitu yao zitakaporejea makwao.

**36.TALIB: (Laughing)** Na nadhani inatubidi kuyapamba maelezo HAYO vizuri, dadangu!

**37.CHIKA: (Laughing)** Ndiyo hivyo! Ebu! **(slapping hands)** Nipe tano, ndugu yangu!

**<u>38.MUSIC UP</u>**

## Scene 4

**39. SFX Daytime ambience**

**40.MULOGO:** Baba, nitaongoza kikao kijacho cha usimamizi wa misitu. Utanichorea ardhini ramani ya msitu wa Wilaya ya Abanto? Ningependa kila mtu aitazame na kutoa maoni yake.

**41.CHIEF APALOO:** Naam. Nitafanya hivyo! **(groans)** aaaa! Mgongo wangu. Aaakh! Tangu hapo mimi si mtu ninayeweza kuinama!

**42.MULOGO:** Haya! Kiti hiki!

**43. SFX: Moving Chair**

**44.CHIEF APALOO: (groaning)** Asante, mwanangu! Bora hivyo.

**45.MULOGO:** Hiki kijiti. Kwa hisani yako chora vitu vyote unavyokumbuka vinavyohusu msitu – mipaka yake, maeneo ya makazi, mito, barabara, vijia..

**46.SFX: STICKS SCRAPING IN SAND**

**47.CHIEF APALOO: (Breathing heavily)** Aaa Mulogo! Nimeshamaliza!

**48. SFX; Scraping sounds**

**49.CHIEF APALOO: (Stretching/ groaning)** Na vijiwe hivi vinaashiria vijiji.

**50.MULOGO:** Ni kiasi hekta ngapi? Ukikisia?

**51.CHIEF APALOO:** Eneo zima ni kama hekta elfu mia moja. Kutokana na wadhifa wangu wa chifu nilikuwa na nyaraka rasmi zilizoonyesha maeneo yote ya mwitu na nani walioyamiliki.

**52.MULOGO:** Lakini endapo misitu yetu na vijiji vyetu vimeharibiwa na vita, basi takwimu hizi si sawa.

**53.CHIEF APALOO:** Na pengine hizo nyaraka pia zimeharibiwa.

**54.MULOGO:** Wataka kusema kwamba serikali itakosa nakala? Itabidi tuulize. Kulingana na hati ya nyanjani ya *Saidia Afrika*, hatua muhimu ya kwanza katika usimamizi wa misitu ni kujua wanaomiliki ardhi inayohusika.

**55.CHIEF APALOO:** Kweli, wakati shirika la FARM litakapoanzishwa kikweli, watatupa hizo taarifa.

**56.MULOGO:** Njoo, baba! Tumalize kuchora hii ramani ardhini, kisha tutakuwa tumepambaukiwa na hali ya mambo ilivyo kabla ya mkutano.

**57.CHIEF APALOO:** (Proudly) Una kipaji cha uongozi, mwanangu! Ninajivunia kuwa na mtoto kama wewe!

**Scene 5**

**58. SFX Daytime ambience**

| | |
|---|---|
| **59.ISI:** | Akiki, ningependa kumuuliza Sesi yaliyowapata ndugu zangu, hususan Kato. Nahisi kama anajua kitu. |
| **60.AKIKI:** | Isi, mbona unataka kujiumiza moyo? Hawezi kukuambia. Hawezi kutamka neno lolote. |
| **61.ISI:** | Lakini juma lililopita ulisema hali yake inaimarika. |
| **62.AKIKI:** | Ndiyo, pindi Chifu Apaloo anapomsimulia moja wapo ya hadithi zake za misitu. |
| **63.ISI:** | Una maana kwamba alighumiwa na mambo aliyoyaona miezi kadha iliyopita? |
| **64.AKIKI:** | Naam. Bila shaka alishuhudia mambo ya kutisha. |
| **65.ISI:** | Lakini nina swali moja nitakalo kumuuliza. Swali moja tu. Ninataka kujua. |

**66. MUSIC UP AND FADE**

**Scene 6**

**67. SFX Daytime ambience**

**68.MOTHER:** Karibuni kwenye kikao cha FARM- mkutano wetu mpya wa kundi la usimamizi wa misitu nyanjani.

Hatua ya Pili: Usimamizi wa misitu. Zamu ni yako Mulogo!

**69.MULOGO:** Hamjambo. Tuanze kwa kutizama ramani ya msitu wetu ambayo imechorwa na babangu Chifu Apaloo hapa ardhini. Tafadhali karibieni. Itizameni vizuri!

**70.SFX Footsteps…voices approving.**

**71.THEMBA:** Na vipi kuhusu msitu wetu Banega?

**72.MOTHER:** Naam, wilaya yetu inapaswa kujumuishwa.

**73.MULOGO:** Ndiyo. Kama mnavyoona, huu hapa mpaka. Hatuna taarifa zenu. Mnatakikana muongeze taarifa hizo nyinyi wenyewe.

**74.CHIKA:** Ni vyema pia tujadiliane ikiwa tunataka kuanzisha msitu wa kijamii ambao tutakubaliana kuusimamia pamoja na tuondoe baadhi ya hii mipaka.

**75.CHIEF APALOO:** Nadhani tunapaswa kuitambua miti tunayotaka kuilinda kwa sababu ya faida tunayopata- kuni, matunda, njugu, mbegu.

**76.MULOGO:** Mbona tusijadiliane kuorodhesha vitu hivyo kulingana na thamani yake! Kwa mfano, tunahitaji dawa, kuni, nyuki. Vitu hivyo vinatuletea kipato.

**<u>77.VOICES APPROVE</u>**

**78.TALIB:** Tunaweza kutayarisha jedwali linaloonyesha misimu na miti na faida zake. Tukiweka taarifa hiyo vizuri, ndipo tutakapojua miti gani inayotakikana kulindwa kwa hali yoyote ile.

**79.MOTHER:** Nafikiri waganga wa miti shamba wanapaswa kushirikishwa. Wana uzoefu wa muda mrefu.

**80.THEMBA:** Mganga wangu wa miti shamba alikosa dawa ya mti ya kumpa mwanangu aliyekuwa akisumbuliwa na minyoo.

**81.CHIEF APALOO:** Themba, usemavyo kweli. Hata hivyo baadhi ya hao waganga wenyewe wamekuwa wakiitumia vibaya mimea ya dawa. Wanapaswa kushirikiana nasi kupanda tena miti wanayoikata kwa dawa..

**82.MULOGO:** Na pia wenye biashara za mbao wanatakikana kujitokeza. Wanafaa kushirikiana nasi kuamua miti ya kukata, na kupanga miti gani ambayo inaweza kukatwa kwa usalama. Hakuna atakayefaidika ikiwa miti itakatwa zaidi kiasi cha kutoweka kabisa. Hakuna jingine la kufanya ila hivyo!

**83.CHIKA:** Maanake huo ndio usimamizi wa misitu.

**84.SFX: PAPER NOISE**

**85.MULOGO:** Sasa, nitawasambazia karatasi hizi zenye majedwali. Jiungeni kwenye vikundi kisha muanze kujaza. Muongeze maeneo mjuayo kwenye ramani iliyoko ardhini na mkimaliza nitachora kila nitakachokiona kwenye bango ili kila mtu ashuhudie.

**86. APPROVING VOICES**

**87.CHIEF APALOO: (Softly)** Simwoni Isingoma hapa, Mama Kipko.

**88.MOTHER: (worried)** Kweli. Yeye si mtu wa kukosa kuhudhuria mikutano.

**89.CHIEF APALOO:** Hivi ninaondoka. Nakwenda kumtazama Sesi nione kama Isi yuko huko.

**90.MOTHER:** Nakushukuru, Chifu Apaloo. Unamchangamsha msichana. Masikini mtoto wa watu! Nasubiri siku atakayorejelewa na uwezo wa kusema..

**<u>Scene 7</u>**

**<u>91. SFX Daytime ambience</u>**

**<u>93.SFX. DISTANT SOUND OF ISI CRYING. KNOCK ON DOOR</u>**

**94.CHIEF APALOO:** Isi? Mwanangu, una nini?

**<u>95. SFX: OPENING OF DOOR</u>**

**96.ISI: (sniffing in tears)** Oh Chifu Apaloo, nimwelezeje mamangu?

**97.CHIEF APALOO:** Mbona? Kwani nini kimetendeka?

**<u>98. SESI WHIMPERING</u>**

**99.CHIEF APALOO:** Sesi! Hujambo mwanangu. Kuna nini?

**100.ISI:** Ameweka siri nyingi.

**101.CHIEF APALOO:** Siri? Vipi? Siri gani?

**102.ISI: (sobbing)** Hawezi kuzungumza! Inasikitisha zaidi! Lakini ameniashiria kwa mikono…**(bursting out loudly)** Kato hayuko hai tena!

**103.CHIEF APALOO:** Oh pole. Pole sana mwanangu.

**<u>(COMFORTS ISI)</u>** Shhh. Shhh.

**<u>104.SESI WHIMPERS SOFTLY</u>** Hmmm

**105.CHIEF APALOO:** Sesi mwanangu. Njoo. Jifunike burangeti hili.

**106.CHIEF APALOO:** Akiki yu wapi?

**107.ISI: (sniffing)** Ameondoka na ng'ombe wake Kiroko kwa malisho.

**108.CHIEF APALOO**: Acha nende kumwita mamako.. Isi, nenda kamtafute Akiki. Sesi. Nawe ubaki hapa. Tutakutana hapa hivi punde. Mama Kipko anafaa kufahamishwa.

## Scene 8

**110. SFX Daytime ambience. Cows**

**111.AKIKI: (talking softly)** Kiroko, hakuna mwingine anayejua. Hata mmoja. Ni mimi tu na dadangu. Nilijua kuhusu mti wa mbuyu. Ninajua siri nyingine. Mimi pekee. Dadangu aliushika mkono wangu akauweka hapo, kwenye tumbo lake. Ninajua maanake Kiroko! Nilihisi joto kwenye mkono wangu. Ai! Ai! Na ni mimi tu ninayejua nani ndiye baba.

**112. MUSIC UP**

**OUTRO.**

Ni hayo tuliyokuandalia kwa leo katika kipindi cha *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* kiitwacho "Mti unapoanguka...", kilichoandikwa na Romie Singh, kinachoshughulikia suala la uharibifu wa misitu.

Kazi ya shirika la FARM imeimarishwa. Lakini je Sesi atawahi kuzungumza tena? Atasema lililompata Kato, ndugu pacha wa Isingoma? Usikose kujiunga nasi katika kipindi cha mwisho upate kujua mambo yatakavyokuwa.

Kumbuka, ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki au kuwaarifu marafiki zako kukihusu, tafadhali tazama wavuti wetu www.dw-world.de/lbe

Kwaheri kwa sasa!

**END OF EPISODE 9**